

# MIUNGANISHO

**Bishop Middle School** wanafunzi wa darasa la nane wanapokea vyeti vyao vya kupiga hatua wakati wa Sherehe yao ya Kupiga Hatua katika PCTA. HONGERA

JUNI 28, 2023

## KONA YA AFISA MKUU MSIMAMIZI

Karibu kwenye toleo jipya la Shule ya Umma ya Wilaya ya Providence (PPSD) kijarida cha mara mbili kwa wiki! Ninafurahia sana kutangaza kwamba tulikuwa na mahafali ya shule ya sekondari wiki iliyopita, ikiwa na wanafunzi zaidi ya 1 000 wakivuka jukwaa kupokea diploma zao. Hongera kwa kila mmoja wenu kufikia hatua ya mwisho. Uli stahili hii. Pia, hongera kuu wa wanafunzi wetu wote wa darasa la nane ambao walikuwa na sherehe zao za Kupiga Hatua.

Katika mahafali wili iliyopita, tuli vumbua mpango wetu wa kusoma msimu wa joto. Kabla ya kufunga shule, tuli safirisha vitabu 90 000 vilivyo ambatana na umri kwa wanafunzi wote wa Pre-K hadi Darasa la 5.  Pia tuli pokea matembezi kutoka Clifford Mbwa Mkubwa Mwekundu katika Messer Elementary School kama mpango wa kusoma msimu wa joto.



DKT. JAVIER MONTAÑEZ
AFISA MKUU MSIMAMIZI

Pia ni wiki kubwa kwa wanafunzi wetu wa CTE. Wengi walitia saini makandarasi na kampuni 14 kutoka jimboni kote kuanza taaluma zao baada ya kuhitimu kutoka shule ya sekondari. Ninajivunia kuhusu kiwango cha wanafunzi walio fanya vyema katika mpango wa CTE katika shule zetu za sekondari, na wameamua kupiga jeki taaluma zao. Tunawatakia kila la heri wakati munapoanza safari katika kazi.

Majira ya Joto yenye Furaha! Toka nje, furahia hali ya anga, na soma, soma, soma!

## WEKA ALAMA KWENYE KALENDA ZENU!

- **SIKU YA KWANZA YA MPANGO WA MASOMO YA MAJIRA YA JOTO**
  Jumatatu, Julai 10
- **SIKU YA USHINDI**
  (Hakuna Mpango wa Majira ya Joto)
  Jumatatu, Agosti 14
- **SIKU YA MWISHO YA MPANGO WA MASOMO YA MAJIRA YA JOTO**
  Alhamisi, Agosti 17
- **MAENDELEO YA KITAALUMA KWA MWALIMU**
  Jumatatu - Alhamisi, Agosti 28 - 31
- **UELEKEZO WA MWALIMU**
  Jumanne, Septemba 5
- **SIKU YA KWANZA SHULENI**
  Jumatano, Septemba 6

# TAARIFA MPYA ZA WILAYA







## MIPANGO YA MASOMO YA MAJIRA YA JOTO YANAANZA JULAI 10!

Shule zinaweza kuwa zimefungwa, lakini Mipango yetu ya Masomo ya Majira ya Joto yako karibu kuanza kikamilifu! Tuko na zaidi ya wanafunzi K-12 zaidi ya 1 500 walio jisajili kushiriki katika mipango yote Wilaya inataka kupeana kuanzia Julai tarehe 10 hadi Agosti 17. Mipango hii inajumuisha:

**Summer Stars Learning Academy**
**Madarasa K-8**
**Jumatatu - Ijumaa, saa mbili asubuhi hadi saa kumi na moja jioni 8:00 a.m. hadi 5:00 p.m.**
***Young Woods Elementary School &***
***Alfred Lima Elementary School***

Wakati wa mpango huo, wanafunzi wataboresha ujuzi wao katika kusoma, kuandika, na hisabati na hata pia kushiriki katika kipengele cha kuvutia cha hisia kuvutia watoto na wahisi wame jumuishwa! Wanafunzi watajenga imani na kufanikiwa katika masomo yao kwa kusoma kwa bidii, kushiriki na marafiki, na kusoma ujuzi wa msingi ambao utawabeba kupitia mwaka wao wa shule na zaidi!

**STEM katika DelSesto**
**Madarasa 6-8**
**Jumatatu - Alhamisi, saa mbili asubuhi hadi saa nane jioni 8:00 a.m. hadi 2:00 p.m.**
***DelSesto Middle School***

Mpango wa masomo ya majira ya joto ya middle school, wanafunzi wanachagua uchaguzi tatu, SeaPerch, NEED, au E-Michezo. Katika SeaPerch, mpango wa robotiki wa STEM, wanafunzi wanapata uzoefu wa dhana ya utangulizi wa uhandisi na kupata uzoefu halisi ukijumuisha mashindano ya uundaji wa boti. NEED ina angazia shughuli za STEM iliyoundwa kwa wanafunzi kuona dunia halisi na kujenga mahusiano kuhusu Sayansi Nyuma ya Elimu ya NISHATI. Katika E-Sports, Michezo ya Kieletroniki, wanafunzi wanapata usaidizi wa ujuzi hali wa karne ya 21 ikijumuisha kuwaza kwa umakini. E-michezo inakuwa kwa kasi sana katika mashindano ya shule za sekondari huko Marekani, na na mchezo huo ume ambatanishwa na Ligi ya Michezo ya Rhode Island (RIIL). Je unapendelea kujiunga na mpango wa middle school? ***Jisajili hapa***!

**Shule ya Sekondari ya PPSD Urejeshi wa Alama Majira ya Joto**
**Madarasa 9-12**
**Jumatatu - Alhamisi, saa mbili asubuhi 8:00 a.m. hadi saa nane jioni 2:00 p.m.**
***Central High School***

Mpango huu utatumia jukwaa la mtandaoni la Edgenuity na kuchanganya masomo mtandaoni pamoja na mafundisho ya mwalimu, kazi za vikundi na miradi. Madarasa halisia kama elimu ya mazoezi na sanaa zita fundishwa katika muundo wa madarasa ya kawaida.




# USAWA NA USHIRIKI

**RESPECT Akademia ya Uongozi**

**Jumatatu, Agosti 14, 2023 - Ijumaa, Agosti 25, 2023**

**Eneo:** Chuo kikuu cha Brown

**Hadhira:** Wanafunzi wa PPSD Middle & High School

*Bila malipo kwa wanafunzi ambao wamekuwa washiriki amilifu katika RESPECT. Kiamsha kinywa, chakula cha mchana na vitafunio vitatolewa. Wanafunzi watapata posho. Jisajili hapa.*

**Baraza la Ushauri la Usawa** Mkutano huu wa mwisho la Baraza la Ushauri la Usawa lilifanyika leo, Juni tarehe 28. Tunashukuru sana washirika wetu kwa kazi yao ya bidii na hususan kazi yao ya bidii kurekebisha Rangi na Sera ya Usawa Kikabila iliyopitishwa na Bodi ya Shule mnamo Juni tarehe 21. Ikiwa ukipenda kujiunga Baraza tafadhali tuma barua bebe equity@ppsd.org.

**Timu ya Uongozi wa Usawa Mabalozi Viongozi:** Tunatafuta walimu wawili kutoka kila elementary, middle na high school, kushiriki katika mpango ulioundwa kipekee kwa mafunzo ya uongozi. Ilikusudiwa kutayarisha washiriki kuhudumu kama Timu ya Uongozi wa Usawa Mabalozi Viongozi. Mafunzo haya yatalingana na ujumbe, *Vitendo Vitano vya Uongozi Unao lenga Usawa*, na itawezeshwa na mwandishi mmoja, Dkt. Mark Gooden. Kama Mabalozi Viongozi, hawa watu watatengeneza na kuongoza timu za uongozi katika shule zao, wakati wa mwaka wa shule 2024-25. Ikiwa wewe ni mfanyakazi wa miezi 12 na ungependa kushiriki katika kazi hii, tafadhali ongea na mwalimu wako mkuu au wasiliana na Ofisi ya Usawa na Ushiriki katika *equity@ppsd.org*.

---



## MAISHA YA BAHARINI KAMA SANAA

**Webster Avenue School** wanafunzi wa darasa la tatu walishiriki na msanii na msaidizi wa mwalimu kutoka Shule za Umma za Providence, **Nilton Cardenas**, katika mradi wa sanaa ya maisha ya baharini. Kila mwanafunzi alichagua mnyama wa bahari kufanya utafiti na kutengeneza mchanganyiko wa mnyama huyo ndani ya maji. Cardenas alishiriki pamoja na Sodexo kutengeneza sanaa katika 797 Cafe katika Shule za Umma za Providence Ofisi ya Central. Wanafunzi na msanii waliandaa maonyesho ya sanaa katika cafe Juni tarehe 20.



# KUWASHEREHEKEA WANAFUNZI

Wanafunzi wetu wenye bidii na wenye talanta wanafanya mambo mazuri kila siku. Hapa kuna mifano michache.




## SHEREHE ZA KUPIGA HATUA

Hongera kwa wanafunzi wetu wote wa chekechea, darasa la 5, na darasa la 8 ambao walisherekea **Sherehe za Kupiga Hatua** katika wiki mbili zilizopita! Wanafunzi walisherekea mafanikio yao wakati wa muda wao shuleni na kusherekea kuendelea na safari yao ya masomo. Tunangojea kwa hamu kutazama yote mutakayo tekeleza wakati munapo endelea na hatua yenu nyingine ya kimasomo!



## MOUNT PLEASANT INANG'AA KATIKA OLIMPIKI SPESHELI

Mapema mwezi huu, washiriki wa Timu ya Kuinua Chuma Mount Pleasant Kitties alishinda medali za dhahabu 4 na medali za fedha 11 katika Deadlifti na Msukumo wa Benchi katika michezo ya Olimpiki Spesheli 2023 iliyofanyika katika Chuo kikuu cha Rhode Island. Zaidi na hayo, mwanafunzi wa darasa la chini MateoMilagro Oliver, mshiriki wa timu, alichaguliwa kuwakilisha Wilaya na timu katika kupitisha tochi wakati wa sherehe ya ufunguzi! Shukrani maalum kwa wakufunzi Louie Stravato na Katherine Gonzalez, Mwalimu Spesheli wa Mount Pleasant , na hata pia wataalamu wa jumuiya, na wazazi waliojitolea ambao walikuja kushangilia wanamichezo!




## MASHUJAA YA MAHUDHURIO

Shukrani kubwa kwa **New England Patriots** na **Kraft Foundation** kwa kurudi kwa **Young Woods Elementary School** kusaidia kusherekea Mashujaa wetu wa Mahudhurio! Patriots wako hapo pia kusaidia kufanya wanafunzi wapate msisimko kuhusu masomo ya msimu wa joto. Kila mwanafunzi aliweza kuleta nyumbani vitabu vitabu vya kusoma! Wanafunzi wetu walitokea katika video ya Patriots kwenye mitandao ya kijamii unaweza kutazama hapa: *https://twitter.com/i/status/1670831556397789190*



## MOUNT PLEASANT BESIBOLI INA FAGIA KUSHINDA RIIL MASHINDANO YA DIVISHENI III

Hongera kwa timu ya **Mount Pleasant Kilties Besiboli** kwa ushindi wa 5-0 juu ya Exeter-West Greenwich katika ufagio wa mchezo 2 kwa Mashindano ya Besiboli RIIL Divisheni III mwezi huu! Waliweka mchezo wakfu kwa ukumbusho wa mwanafunzi wa besiboli wa kale wa Mount Pleasant Wilcar Moreno.



## WANAFUNZI WA PCTA HUKO ATLANTA KWA SKILLSUSA

Kazi nzuri katika **Elimu ya Kazi na Ufundi** (CTE) wanafunzi ambao walikuwa Atlanta kwa **Kongamano la SkillsUSA Uongozi wa Kitaifa na Ujuzi**! Hongera kwa **PCTA** wanafunzi wa ujuzi wa urembo **Briana Lopez**, **Stephanie Ramos** na **Crystal Aguilar** ambao walishinda medali za dhahabu katika mashindano ya kitaifa katika Kongamano la SkillsUSA Uongozi wa Kitaifa na Ujuzi! Hongera kwa Mshauri mwenye talanta **Stephanie Accetta** na mwalimu **Bi. GomesMcCreary**! Hongera pia kwa **Karriana Phoeun**, **Emelie Rosa**, na **Melanie Rosa**, wa Njia ya Taluma kwa mpango wa Huduma za Binadamu pamoja na Bi. GomesMcCreary, aliyekuwa wa 6 nchini! Pia tungependa kutambua mwanafunzi wa darasa la juu anayepanda **Winifer Rodriguez** waliochukua nafasi ya 5 kwa mashindano ya upishi. Asante, **Mpishi Rodriguez**, kwa kufanya kazi kwa bidii! Hongera kwa mwanafunzi wa darasa la chini anayepaa **Fritz Heitmueller** aliyechukua nafasi ya 10 nchini katika Magari ya Viwanda na udhibiti pamoja na usaidizi kutoka walimu wa Teknolojia ya Umeme **David Santos** na **Robert Gianfrancesco**!

## TUZO LA MCHEZAJI MASHUHURI

Hongera kwa **Gilbert Stuart Middle School** mchezaji wa mpira wa kikapu **John Ramos** kwa kushinda Tuzo la Mchezaji Mashuhuri katika Kitengo cha Wavulana kwa Ligi ya Mpira wa Kikapu katika Providence Middle School! Tuzo lilipeana kwa John kupitia mkufunzi wake na Afisa mkuu msimamizi Montañez.



# NI HABARI NJEMA: PPSD KWENYE VYOMBO VYA HABARI

- Je, Shule za Umma za Providence zinapaswa kutumia vipi $ 100 000? Hii ni juu ya hawa wanafunzi wa middle
  *Brown News*, Juni 8, 2023
- Kama sehemu ya mpango wa mwaka mmoja, wanafunzi wa Providence watapokea dakika 30 za ziada katika muda wa masomo
  *ABC6*, Juni 16, 2023
- Shule za Umma za Providence zitakuwa na siku ndefu ya shule mwaka ujao. Hivi ndivyo itakavyo kuwa.
  *Jarida la Providence*, tarehe 16, 2023 Juni
- Pre K-Gr. Wanafunzi wa 5 wa Providence watapewa mkoba pamoja na vitabu 10 kwa masomo ya majira ya joto
  *RI News*, Juni 17, 2023
- Imehamasishwa kupitia Makumbusho ya Moreno, Mt. Pleasant Inakamilisha Divisheni III Ufagio wa Mashindano ya Mpira wa Kikapu
  *ABC6*, Juni 18, 2023
- Hope High School una vumbua ukumbi mpya ulio rekebishwa
  *WPRI*, Juni 21, 2023
- Jimbo, viongozi wa maeneo wanakata kitambaa katika ukumbi mpya wa Hope High School
  *ABC6*, Juni, 21, 2023




# KUANGAZIWA KWA MWANAFUNZI

Wajue wanafunzi wetu hodari wa darasa la juu Wilayani!

**Favoured Adeoye**
*Mwanafunzi wa darasa la juu, JSEC*
MS: Baltimore, MD
ES: Nigeria

**Blessed Adeoye**
*Mwanafunzi wa darasa la juu, JSEC*
MS: Baltimore, MD
ES: Nigeria

***Tuliambiwa kwamba nyinyi ni mapacha. Nani kati yenu ndio mkubwa na nani ndiye mwanafunzi bora zaidi wa kwanza?***

**FA:** Mimi ndiye pacha mkubwa na pia mwanafunzi bora zaidi wa kwanza. Hadithi ya kuvutia, Blessed alipata COVID na alama zake zika didimia kidogo katika mmoja ya madarasa yetu ambapo nilipata alama ya A. Mwishowe, yeye alikuwa mwanafunzi bora wa pili nami nikawa mwanafunzi bora zaidi wa kwanza.

***Mipango yako ni gani baada ya kuhitimu?***

**FA: Napanga kwenda chuo kikuu cha Roger Williams na nitafuata mkondo wa uhandisi. Katika miaka chache ya kwanza nitafuata mkondo lakini baada ya miaka miwili, nawaza kulenga uhandisi wa mashine ya umeme. Ni mpango wa kidesturi kwa hivyo unaweza badilisha uhandisi wa urai au uhandisi wa kimatibabu na kibiolojia. Tulichagua shule hiyo baada ya kukutana na mwanafunzi wetu wa awali katika kanisa letu. Alitukaribisha kuja na kutazama Roger Williams. Tuliweza kuona shule katika siku ya kawaida na kuongea na wanafunzi kadhaa. Tuliipenda sana.**

**BA: Hata mimi pia nitaenda Roger Williams. Napanga kufanya utaalamu kwa uhandisi wa umeme. Pia nawaza kuwafanya utaalamu maradufu na kusoma usimamizi wa biashara. Tuko tayari kwenda shule tofauti lakini Roger Williams ulitupunguzia bei ya undugu na juu yake kutupatia usaidizi wa kifedha mwingine. Sababu kuu nilitaka kwenda Roger Williams ni kwa sababu ni shule nilihisi nimeungana nayo sana. Ilikuwa na chuo cha kupendeza na ilionekana kama italeta uzoefu bora zaidi kusoma kupitia profesa wote tulio kutana nao. Sote tulipokea Ufadhili wa Masomo wa Raisi. Tulipata ruzuku za ziada na ufadhili wa masomo.**

> “Baada ya COVID, niliepuka watu sana. [Bw. G daima alisema aliona sifa za uongozi kwangu...daima nitashukuru kwa hiyo. Sasa, daima niko tayari kujitetea.” - Blessed Adeoye

***Kwa nini ulichagua JSEC?***

**BA: Tuli hamia mara moja hadi Rhode Island kutoka Baltimore baada ya darasa la 10. Ilikuwa mchakato mzima wa kuchagua ni sehemu gani tutakapo kwenda. JSEC ilikuwa kama matembezi ya dakika tano kutoka nyumbani. Tumefurahia muda wetu hapa na tuka patiwa fursa nyingi. Tumegundua kuhusu mpango wa kuharakisha wa TayarishaRI. Kama sehemu ya mpango, sote tunaweza kufanya mafunzo ya kazi katika Amgen, kampuni ya dawa za kibiolojia, wakati wa majira ya joto. Ilikuwa mafunzo ya kulipwa. Tuliweza kujiunga na jumuiya ya heshima pia.**

**FA: Mpango wa TayarishaRI ni wa wanafunzi wa darasa la juu kutumia mwaka wao mzima wa darasa la juu katika Chuo cha Jumuiya katika Rhode Island (CCRI). Bado unaweza kushiriki katika michezo na shughuli shuleni mwako lakini kwa msingi unatumia mwaka wako wote wa darasa la juu kwenda chuoni. Wewe ni kama mwanafunzi wa mwaka wa kwanza chuoni. Unachukua madarasa nne kwa muhula. Mpango ulitupatia fursa kuchukua madarasa na kupata takriban mwaka mbele wakati wa kuingia chuoni. Sote tuna chagua mkondo wa uhandisi. Tulipata uzoefu chuoni na kuona vile itakuwa. Tumekuwa na washauri katika CCRI. Kulikuwa na wanafunzi 68 PPSD waliofanya mpango mwaka huu katika shule zote za PPSD. Tunapaswa kutengeneza urarifki mzuri na wa kudumu katika mpango. Mazingira ya CCRI ulikuwa wa kirafiki. Ilibidi uwasilishe ombi na ukubaliwe. Inabidi upendekezwe kupitia washauri wako na kuwa na kiwango cha chini cha GPA.**

Je, kumekuwa na mwalimu ambaye amekuwa na athari katika maisha yako katika JSEC?

**BA: Mwalimu aliyekuwa na athari kubwa kwangu alikuwa**

*ukurasa. 6, kuendelea kwa Kuangaziwa kwa mwanafunzi*

**Bwana Malone au kama nilivyo mwita "Bwana. G." Alikuwa mwalimu wangu wa Kiingereza, na alikuwa mtu aliyenisaidia kuanzia mwanzo. Alitambua mapema mambo mengi ya msingi kutoka shule yetu ya awali, kwa hivyo tuko tayari kuchukua kazi zenye changamoto zaidi na kutu sukuma kufanya zaidi. Pia alinihimiza kutoka nje ya gamba langu. Baada ya COVID, niliepuka watu sana. Kwa hivyo, kuja kwa shule hii ilikuwa uzoefu wangu nje ya hiyo. Daima alisema kwamba aliona sifa kuu za uongozi ndani yangu, na hakutaka zipotee. Daima alijaribu kunisukuma na daima nitashukuru hiyo. Sasa, daima niko tayari kujitetea.**

**FA: Mwalimu aliyekuwa na athari kuu kwangu alikuwa Bi, Martha Heald. Alinifundisha utangulizi wa hesabu. Amestaafu sasa. Wakati tulipokuja kutoka Baltimore, tulikuwa mwaka mmoja mbele ya darasa lote. Alifanya bidii ya ukweli kuwasiliana nasi na kutu jumuisha. Alisomea uhandisi wa uraia. Alipotambua ninapendelea uhandisi, alinisaidia kufanya utafiti wa shule. Alinisaidia kupata uzoefu shuleni wakati tulipo hamia kwanza hapa. Pia alinisaidia kuona kwamba hisabati inaweza kufurahisha. Na mpaka leo naongea naye.**

***Tukio lako la kukumbukwa zaidi kutoka shule ya sekondari ni gani?***

**FA: Ningesema ni darasa la Bi. Heald. Kutoka Baltimore, hatukuwa karibu na chakula cha Kidominika. Tulijaribu Mangu, lishe ya Kidominika, kwa mara ya kwanza katika darasa lake. Ilikuwa nzuri. Ilinifungua kwa watu wengine katika darasa langu na kuthamini tamaduni zingine. Ilikuwa kwa wiki ya utamaduni.**

**BA: Kumbukumbu yangu bora kutoka mwaka wangu wa darasa la chini ni wakati tulifanya mradi wa Kizazi cha Uraia. Siku tulipoenda ikuluni mwa raisi na kufanya maonyesho ilikuwa uzoefu mkuu. Tulihitaji watu wanne kwenda ikuluni na kufanya maonyesho ya mradi huo. Ilikuwa mara yangu ya kwanza kutoka nje ya gamba langu. Tulifanya maonyesho kuhusu taka na kuchakata taka katika shule na jijini. Tuliwasilia maseneta wetu kuhusu kuweka pipa zaidi za kuchakata taka na uchagunzi katika jumuiya. Tulisukumia kwa vichocheo kwa watu kuchakata taka zaidi. Nahisi kwamba ilibidi nichukue jukumu la uongozi. Sote tulikuwa watu wenye haya, na sikutaka hiyo kuathiri kazi zote tulizo fanya. Kwa hivyo, nilijisikuma na kusukuma wanafunzi wenzangu kufanya maonyesho ya mradi wetu na kuwa wajasiri.**

***Una wasiwasi au una shauku gani baada ya kuhitimu?***

**FA: Nina msisimko kuona jinsi uzoefu wangu katika CCRI utanisaidia kati ya marika wangu. Vidokezo na ushauri mwingi ambao washauri walikuwa wanatupatia katika siku ya maelekezo kwa Roger Williams yalikuwa mambo sawia tuliyojifunza tayari mwaka uliopita. Mara kwa mara, nilihairisha wakati wa mpango na nilijutia. Mwaka huu uliopita, nilijifunza mapema jinsi ya kusimamia mradi na kujaribu kudhibiti vyema kazi yangu. Ilibidi ni pange na kujipatia kasi. Wanafunzi wengi wenzangu walikuwa wa mwaka wa kwanza chuoni.**

**BA: Jambo ninalo hisi hisia zote ni kuhusu Kujidhibiti kikamili. Ingawa tulikuwa na uzoefu wa chuo, hatukuwa na uhuru mwingi. Bado tulikuwa na washauri ambao walitufuatilia kila Ijumaa. Kwa hivyo, tuli saidiwa kuwa katika njia ifaayo. Sasa tukiwa peke yetu, itanibidi nichukue msukani mwenyewe kufanya mambo yangu yote na kujipanga. Pia natarajia kufanya michezo kadhaa pindi ninapofika shuleni. Ningependa kucheza mpira wa kikapu wa ndani ya chumba.**

# WILAYANI



## KUTAMBUA WASHIRIKA WA BARAZA LA USHAURI LA WAZAZI

Shukrani washirika wa Baraza la Ushauri la Wazazi (PAC) **Elaine Faber Budish** na**Tomoko Shibusawa** kwa kujitolea kwao katika Shule za Providence na wanafunzi wetu. Tunashukuru sana muda wako na bidii yako ya dhati mwaka huu uliopita. Wote walitambulika katika mkutano wa Bodi ya Shule. Asanteni tena kwa yote muliofanya kwa Wilaya!




## KUHESHIMU MSHIRIKI WA BODI YA SHULE MARK SANTOW.

Shukrani kubwa inaenda kwa mshiriki wa Bodi ya Shule aliye hudumu kwa muda mrefu sana, **Dkt. Mark Santow**! Santow ni Profesa Msaidizi na Mwenyekiti wa Historia katika Chuo kikuu cha Massachusetts-Dartmouth, mtaalamu katika historia ya kisasa ya Marekani ya karne ya 20, siasa, historia ya kijeshi, haki za raia na sera za kijamii. Santow ali jiuzulu mwisho wa mwaka wa shule kupata muda mwingi na familia yake. Katika miaka nane iliyopita, ali hudumu kama mshauri mkuu wa wanafunzi wa Providence. Mwaka huu uliopita, alisaidia kuongoza sera ya usawa uliosasishwa wakati alipo hudumu kama mwenyekiti wa kamati ya sera. Ana ahidi ataendelea kushughulika kama mzazi katika Wilaya.



## UKUMBI MPYA WA HOPE HIGH SCHOOL

Sherehe ya kukata kitambaa ilifanyika katika **Hope High School** wiki hii kusherekea uvumbuzi wa marekebisho ya ukumbi. Ukumbi ulioundwa upya ni sehemu ya uwekezaji wa milioni $ 20 katika shule kuhudumia bora wanafunzi wa Hope, wanaofanya mipango ya sanaa ya kuigiza, na jumuiya kubwa. Shukrani maalum kwa **Gavana Dan McKee**, **Meya Brett Smiley**, **Kamishna Angélica Infante-Green**, washiriki wa **Bodi ya Shule**, **Muungano wa Walimu wa Providence**, na washiriki wa jumuiya kwa kuwezesha marekebisho haya kwa wanafunzi wetu.




Bofya hapa kutazama video.

© 2023 Providence Public Schools · communications@ppsd.org · www.providenceschools.org

Mambo ya kusisimua yanatokea katika Wilaya nzima na tunataka kueneza ujumbe! Ikiwa una programu, hafla, Mfanyakazi au mwanafunzi mwenye hadithi nzuri ajabu ambayo ungependa kuonyesha, tafadhali tuma barua pepe kwa communications@ppsd.org.